**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA AFYA YA AKILI DUNIANI

**DODOMA: 10 Oktoba, 2025**

Tarehe 10 Oktoba kila mwaka, Tanzania inaungana na Shirika la Afya Duniani (WHO) pamoja na nchi wanachama katika kuadhimisha Siku ya Afya ya Akili Duniani.

**Kaulimbiu ya mwaka huu ni "Upatikanaji wa Huduma za Afya ya Akili Wakati wa Majanga na Dharura"** ikiwa na ujumbe mahsusi wa kuhimiza huduma za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia na kijamii kutolewa kwa watu wote, hususan walioathirika na majanga kama mafuriko, maporomoko ya ardhi, milipuko ya magonjwa, migogoro, na ajali za barabarani.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), mwaka 2025 watu takribani milioni 305 duniani wanahitaji msaada wa kibinadamu kutokana na migogoro, mabadiliko ya tabia ya nchi, na majanga ya asili. Kati yao, zaidi ya milioni 300 wanahitaji huduma za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia, jambo linaloonesha ongezeko kubwa la mahitaji haya muhimu.

Nchini Tanzania, athari za kisaikolojia zimeonekana wazi wakati wa majanga mbalimbali kama mafuriko na maporomoko ya ardhi yaliyotokea Hanang, Mkoa wa Manyara, 2023 ambapo watu zaidi ya 5,600 waliathirika moja kwa moja. Katika tukio hilo, Serikali kwa kushirikiana na wadau iliwafikia watu 3,380 kwa msaada wa kisaikolojia na kijamii. Huduma hizi zimetolewa pia katika majanga mengine kama mlipuko wa COVID-19, Mpox, Marburg, na maporomoko ya majengo.

Serikali imeendelea kuimarisha huduma za Afya ya Akili kwa kuanzisha madawati ya msaada wa kisaikolojia, kuwajengea uwezo wahudumu wa Afya wa ngazi ya msingi, kushirikiana na viongozi wa dini, vyombo vya habari na mashirika ya kijamii katika kutoa elimu kwa umma, na kupambana na unyanyapaa dhidi ya wenye changamoto za Afya ya Akili.

Serikali inatoa wito kwa Watanzania wote kutambua kuwa huduma za Afya ya Akili ni haki ya msingi ya kila mtu. Tuwasaidie wanaokumbwa na changamoto hizi kwa kuwasikiliza bila kuhukumu, kuwahamasisha kutafuta msaada, na kushiriki katika kujifunza kuhusu afya ya akili. Tujenge jamii yenye huruma, matumaini, mshikamano na upendo.

Imetolewa na:

**Dkt. Grace Magembe**
**MGANGA MKUU WA SERIKALI**